

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAISI TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA JIJI LA MWANZA**

SIMU MKURUGENZI : 225 028 501375  
 OFISI ZOTE: 40334  
 FAX: 255 028 500785



S.L.P. 1333  
**MWANZA.**

**20.04.2017**

**T A N G A Z O**

**ZABUNI YA UWAKILISHI WA UKUSANYAJI WA MAPATO**  
**KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018**

**ZABUNI NA. LGA/089/2017-2018/NC/01.**

1. Halmashauri ya Jiji la Mwanza inapenda kuwaalika watu binafsi, makampuni, Ushirika, Taasisi au vikundi vya watu vilivyosajiliwa kisheria wenye nia, uwezo na uzoefu wa kufanya kazi hiyo kutuma maombi yao kwa zabuni hii katika vyanzo mbalimbali vya mapato kama ifuatavyo:-

Na.	Maelezo <i>[orodha ya kina, ya maelezo ya mahitaji/viwango na vipimo]</i>	FUNGU YA KUTOLEA ZABUNI
<b>Uwakala wa ukusanyaji wa Mapato kwenye vyoo vya umma</b>		
1.	CHOO SOKO KUU,	ZABUNI NA. LGA/089/2017-2018/NC/01./01
2.	CENTRAL BUS STAND (TBS),	ZABUNI NA. LGA/089/2017-2018/NC/01./02
3.	MLANGO MMOJA(M1),	ZABUNI NA. LGA/089/2017-2018/NC/01./03
4.	MLANGO MMOJA(M2),	ZABUNI NA. LGA/089/2017-2018/NC/01./04
5.	MAKOROBOI,	ZABUNI NA. LGA/089/2017-2018/NC/01./05
6.	NYEGEZI T <sub>1</sub> ,	ZABUNI NA. LGA/089/2017-2018/NC/01./06
7.	NYEGEZI T <sub>2</sub> ,	ZABUNI NA. LGA/089/2017-2018/NC/01./07
8.	KAMANGA FERRY,	ZABUNI NA. LGA/089/2017-2018/NC/01./08
9.	NYAMAGANA STADIUM,	ZABUNI NA. LGA/089/2017-2018/NC/01./09
10.	MWADECO.	ZABUNI NA. LGA/089/2017-2018/NC/01./10
11.	SAHARA	ZABUNI NA. LGA/089/2017-2018/NC/01./11
<b>Ushuru wa Kushusha na Kupakia:-</b>		
1.	Soko la Mlango mmoja, Kata ya Mbugani na Mabatini Mashineni,	ZABUNI NA. LGA/089/2017-2018/NC/01./12
2.	Igoma & Mahina	ZABUNI NA. LGA/089/2017-2018/NC/01./13
3.	Mjini Kati	ZABUNI NA. LGA/089/2017-2018/NC/01./14
1.	Ushuru Mchanga, Mawe, Morumu na Kokoto - Kwa maeneo yaliyoanishwa, Jiji la Mwanza.	ZABUNI NA. LGA/089/2017-2018/NC/01./14
1.	Ushuru wa maegesho ya magari	ZABUNI NA. LGA/089/2017-2018/NC/01./15

2. **Maombi yote ya zabuni yazingatie masharti yafuatayo**
  - i) Nyaraka za zabuni kwa lugha ya Kiswahili zinapatikana kwa Katibu wa Bodi baada ya kulipia ada ya maombi ya Tshs. 100,000/= (Ambayo haitarudishwa) kwa kila chanzo cha mapato ambacho mwombaji lazima akitaje.(kila choo,kanda za Ushuru wa kushusha na kupakia ni chanzo kinachojitegemea).
  - ii) Ombi la zabuni liwe na jina na anuani halisi ya mwombaji, aidha aonyeshe mahali ofisi zake zilipo au anapoweza kupatikana (physical address).
  - iii) Mwombaji aonyeshe mchanganuo wa matokeo ya mapato anayotarajia kukusanya, matumizi anayotarajia kuyafanya na kiasi atakachoilipa Halmashauri kwa mwezi.
  - iv) Zingatia kuwa form ya maombi ya Zabuni inajazwa na kusainiwa na mwenye uhalali wa kisheria (Power of Attorney) katika zabuni hii.Kama ni kampuni(Company)
  - v) Leseni ya biashara na uhalali wa ulipa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) na TIN namba
3. Mwombaji wa zabuni endapo atachaguliwa atahitajika kuleta dhamana ya kufanya kazi (Performance Bond), kwa njia ya Banker`s cheque kutoka banki husika yenye thamani ya malipo ya miezi mitatu ya kiasi alichohaidi kuilipa Halmashauri.(Hi ni kwa wazabuni watakao shinda zabuni hii).
4. Mwombaji aonyeshe vifaa alivyonavyo, idadi ya wafanyakazi na uzoefu wao.
5. Mwombaji awasilishe zabuni Original na nakala mbili (2) endapo maelezo ya original na nakala yatatofautiana Original ndio itatumika kwenye tathmini.
6. Zabuni ijazwe vizuri, iwekwe kwenye bahasha isiyo na maandishi yoyote (Plain) na juu ya bahasha iandikwe, namba ya zabuni, kazi inayoombwa, Original & Copy, Anuani ya mkurugenzi bila kuwekwa alama yoyote.
7. Dhamana ya zabuni: Dhamana ya zabuni (Bid Security) italetwa kwa njia ya Banker`s Cheque ambayo itakuwa ni asilimia mbili (2%) ya marejesho ya miezi mitatu ya kiasi alichohaidi mzabuni.
8. Mwombaji atakayeshindwa masharti haya atakuwa amejiondoa mwenyewe kwenye mchakato mzima wa zabuni.
9. Uongozi haulazimiki kuchagua zabuni yoyote.
10. Zabuni zitawasilishwa kwa Mkurugenzi Mkuu wa halmashauri ya Jiji la Mwanza.
11. Mwisho wa kupokea zabuni ni **saa nne (4)** kamili asubuhi (saa ya Afrika Mashariki) ya tarehe **12/05/2017** siku ya **Ijumaa** katika **ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji zilizopo Halmashauri ya Jiji la Mwanza**. Waombaji au wawakilishi wa waombaji wanaalikwa kushuhudia ufunguzi. Ufunguzi utafanywa mara tu baada ya saa ya mwisho ya kupokea zabuni mbele ya waombaji au wawakilishi wa waombaji waliochagua kuhudhuria ufunguzi huo utakaofanyika katika Ukumbi Mkubwa katika ofisi za Halmashauri ya Jiji la Mwanza.
12. Anuani ya kutuma zabuni hizo ni:-  
**MKURUGENZI**  
**HALMASHAURI YA JIJI LA MWANZA**  
**S.L.P. 1333, MWANZA**
13. Zabuni ambazo zitachelewa kwa muda uliopangwa na zabuni zitakazotumwa kwa mtandao (e-mail) hazitapokelewa.

  
**KIOMONI KIBURWA KIBAMBA**  
**MKURUGENZI WA JIJI**  
**MWANZA.**